# TARGETER WINGS
# KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## GREDI YA 6 - MWAKA WA 2025
## SEHEMU A:
## KISWAHILI LUGHA

Wings 005

**Muda: Saa 1**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha Kiswahili na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30
2. Ukisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

**NAMBA YAKO YA TATHMINI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**
**JINA LA SOMO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali **1 - 30** umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu sahihi.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali chagua jibu sahihi:**

29. Ni ipi kati ya vitenzi hivi si vya ngeli ya **KU-KU**?
    A. Kupika
    B. Kufyeka
    C. Kifaru
    D. Kufua

Jibu sahihi ni C.

**Katika karatasi ya majibu:**

**29.** [A] [B] ~~[C]~~ [D] **30.** [A] [B] [C] [D] **31.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D]

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa **8** zilizopigwa chapa

Call for more exam 0703752217



CamScanner

**Swali la 1 hadi la 5.**

**<u>Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.</u>**

| | | |
|---|---|---|
| **Mwanafunzi (Asha)** | : | Shikamoo Mwalimu. (*Huku akimtazama mwalimu*) nimekuja na mama kama ulivyoomba. |
| **Mwalimu** | : | Marahaba Asha. Karibu sana mama Asha, asante kwa kufika. |
| **Mzazi** | : | Asante sana Mwalimu. Kuna shida gani kuhusu Asha? |
| **Mwalimu** | : | Kwa wiki mbili sasa Asha ameonekana kutofanya kazi za darasani vizuri na pia amekuwa akichelewa kufika shuleni. |
| **Mzazi** | : | Asha, mbona hujawahi kuniambia kwamba kuna tatizo? |
| **Mwanafunzi (Asha)** | : | Samahani mama. Nimekuwa nikichelewa kwa sababu ya kazi nyingi nyumbani na pia sijawa na muda wa kusoma vizuri. |
| **Mzazi** | : | Nitahakikisha anapata muda wa kusoma na atawajibika zaidi. Asante kwa kuniarifu Mwalimu. |
| **Mwalimu** | : | Karibu sana. Ushirikiano wa mzazi na shule ni muhimu sana kwa mafanikio ya mwanafunzi. |

**1.** Wahusika wafuatao ni washirika katika mazungumzo uliyoyasoma,yupi sio mhusika?

A. Mwalimu B. Juma

C. Asha D. Mzazi

**2.** Kwa nini Mwalimu alimwita mzazi wa Asha?

A. Kwa sababu Asha alipata alama za juu

B. Asha hakufika shuleni kwa mwezi mmoja

C. Asha alionekana hafanyi kazi ya darasa na pia alichelewa kufika shuleni

D. Asha alipoteza vitabu vyake

**3.** Asha anasema sababu ya matatizo yake ni nini?

A. Ugonjwa

B. Kazi nyingi nyumbani

C. Kukosa kalamu

D. Kucheza sana



CamScanner

4. Mwalimu alisisitiza nini kwa mzazi wa Asha?

A. Kununua sare mpya

B. Kumwandikisha kwenye shule ya bweni

C. Kutoa adhabu kali

D. Kuwa na ushirikiano kati ya mzazi na shule?

5. Mzazi wa Asha aliahidi kufanya nini?

A. Kununua simu mpya

B. Kumpeleka Asha kijijini

C. Kuhakikisha Asha anapata muda wa kusoma

D. Kumwacha Asha aendelee kama alivyokuwa

**Swali la 6 hadi la 9**

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.</u>**

Amina alikuwa mwanafunzi mwenye bidii sana darasani. Siku moja, baba yake alimnunulia kitabu cha hadithi za Kiswahili kama zawadi kwa sababu ya kufanya vizuri katika mtihani . Siku ya pili Amina alichukua kitabu chake shuleni akiwa na furaha. Alijivunia sana kitabu kile cha Hadithi,lakini alipofika darasani, rafiki yake Halima alimwomba akisome kwa muda mfupi.

Amina alisita, lakini kwa kuwa alimpenda rafiki yake , alimpa. Halima alikisoma na kukifurahia sana, ila kwa bahati mbaya kilikosekana baada ya Amina kukiitisha. Halima alihisi vibaya sana, akalia na kuomba msamaha.

Badala ya kumkasirikia, Amina alimkumbatia Halima na kusema, " ninajali zaidi urafiki wetu kuliko kitabu ." Halima alifurahi na tangu siku hiyo wakawa marafiki wa karibu sana.

6. Amina alituzwa kitabu cha hadithi kwa sababu gani?

A. Kwa kuwa ni siku yake ya kuzaliwa

B. Kwa kuwa alifanya kazi ya mama yake.

C. Kwa sababu alifanya vizuri kwenye mtihani.

D. Kwa kuwa alikuwa mgonjwa.



CamScanner

7. Kitabu alichotuzwa Amina kilikuwa cha aina gani?

A. Hadithi za Kiswahili B. Hisabati

C. Sayansi D. Hadthi za kiingereza

8. Nani aliomba kuazima kitabu cha Amina?

A. Mwalimu B. Dada yake

C. Halima D. Juma

9. Nini kilifanyika baada ya rafikiye kuazima kitabu?

A. Mwalimu alikichukua

B. Kilipotea darasani kwa njia isiyoeleweka

C. Kiliandikiwa hadi kikaisha

D. Kilianguka na kuvunjika

**Swali la 10 hadi la 12**

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.</u>**

Ilikuwa ni usiku wa manane katika Kijiji cha Mvuleni. Watu wote walikuwa wamelala isipokuwa kijana mmoja Jasiri aitwaye Musa. Mara alisikia sauti ya ajabu ikilia kutoka mwituni: "hu- huu…hu- huu..". Musa alishtuka, lakini badala ya kukimbia, alichukua tochi na bastola ya miale (***flare gun***) aliyokuwa nayo kwa ajili ya dharura. Alitembea polepole kuelekea mwituni.

Alipofika karibu na eneo la sauti, Aliona mwanga uking'aa juu ya mti mkubwa. Kulikuwa na ndege mkubwa wa ajabu mwenye macho mekundu. Alikuwa amejeruhiwa kwenye bawa. Sauti aliyokuwa akisikia ilikuwa ya maumivu. Musa alimsaidia ndege huyo, akamfunga bawa na taulo aliyokuwa nayo.

Asubuhi ilipofika , ndege huyo aliruka juu na kutoweka angani huku akiwacha manyoya ya dhahabu ardhini. Tangu siku hiyo, kila usiku wa mwezi mpevu, Musa alipata zawadi ya ajabu mlangoni mwake – matunda ya porini,fedha na wakati mwingine hata mawe ya thamani. Hakufahamu zawadi zile zilitoka kwa nani, lakini alijua urafiki wake na ndege wa ajabu haukuwa wa kawaida.

10. Musa aliishi katika kijiji kipi?

A. Milimani B. Mtoni

C. Mvuleni D. Mwituni



CS CamScanner

11. Musa alichukua nini kabla ya Kwenda msituni?

A. Simu na kisu

B. Tochi na bastola ya miale

C. Chakula na maji

D. Miti miwili na mfuniko

12. Ni nini kilimtokea Musa kila usiku wa mwezi mpevu?

A. Aliota ndoto mbaya

B. Alipoteza vitu vyake

C. Alipata zawadi mlangoni mwake

D. Alisikia sauti tena

**Swali la 13 hadi la 15**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Siku moja, Wanyama wote wa msitu wa Gungumalo walikusanyika kufanya uchaguzi wa mnyama kiongozi wa msitu. Simba, aliyekuwa mzee na dhaifu, aliamua kustaafu. Ilikuwa ni lazima apatikane kiongozi mpya. Wanyama waliopendekezwa walikuwa:

1. Chui – alisema , ' mimi ni mwepesi na Hodari, naweza kuwalinda wote!'
2. Tembo – akasema, ' nina nguvu na kumbukumbu, sitasahau shida zenu.'
3. Kobe – akasema kwa upole ' mimi ni mwenye Subira, naweza kusikiliza kila mmoja.'
4. Paka – alijitokeza na kusema ' mimi ni msafi, nitatunza msitu kama ninavyotunza manyoya yangu.'

Kura zilipopigwa, kilichowashangaza wote ni kwamba Kobe ndiye aliyeshinda! Wanyama wengi walichoka wenye haraka na kelele. Walitaka kiongozi mwenye busara, anayejali na kusikiliza. Chui alikunja mkia, Tembo akatikisa masikio yake kwa mshangao na Paka alifuta vumbi. Kobe alitembea polepole hadi jukwaani na kusema kwa sauti ya utulivu, " uongozi si kukimbia, ni kuelewa na kusuluhisha."

13. Kwa nini Wanyama walikusanyika msituni?

A. Kufanya sherehe

B. Kumchagua mnyama kiongozi wa msitu.

C. Kupigana na simba

D. Kutafuta chakula



CamScanner

14. Ni nani aliyekuwa kiongozi wa zamani wa msitu?

A. Chui

B. Tembo

C. Simba

D. Nyani

15. Kwa nini kobe alichaguliwa kuwa kiongozi?

A. Alikuwa na nguvu

B. Alikuwa mwenye subira na busara

C. Alikuwa mwepesi sana

D. Alikuwa na marafiki wengi

**Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo kati ya yale uliyopewa.**

Nchi ya Kenya imo katika bara la ___16___.Wazalendo wale walipigania uhuru dhidi ya utawala wa ___17___. Chama kilichoongoza mapambano hayo kilikuwa KANU. Kiongozi ___18___ kwanza wa Kenya baada ya uhuru alikuwa ___19___. Kenya ilipata uhuru ___20___ mwaka 1963 .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | **A.** Asia | **B.** Ulaya | **C.** Afrika | **D.** Amerika |
| **17.** | **A.** wafaransa | **B.** waingereza | **C.** wajerumani | **D.** waarabu |
| **18.** | **A.** wa | **B.** ya | **C.** cha | **D.** mwa |
| **19.** | **A.** Jaramogi Odinga | **B.** Jomo Kenyatta | **C.** Kenneth Matiba | **D.** Uhuru Kenyatta |
| **20.** | **A.** yake | **B.** wake | **C.** wao | **D.** yao |

**Kutoka swali la 21 hadi 30, chagua jibu sahihi.**

21. **Ukanusho wa sentensi:**

"Wanafunzi wanasoma vitabu" ni ______________________

A. wanafunzi hasomi vitabu

B. wanafunzi hawasomi vitabu

C. wanafunzi wasingesoma vitabu

D. mwanafunzi anasoma kitabu



CS CamScanner

22. Wakati ujao wa sentensi ifuatayo ni:

**"anakula chakula"**

A. Amekula chakula

B. Atakula chakula

C. Alikula chakula

D. Anakula chakula

23. Wingi wa neno **"jiwe"** ni?_________________

A. Mawe

B. Majiwe

C. Vijiwe

D. Majijwe.

24. Tambua maana ya nahau: Mtoto **alipiga chafya**.

A. Mtoto alipigwa na mwalimu

B. Mtoto alichemua

C. Mtoto alipata taabu

D. Mtoto alikuwa mgonjwa

25. **Chagua jibu sahihi kukamilisha sentensi:**

Pendo alifeli mtihani wake _______________ alikuwa mgonjwa.

A. kwa sababu

B. lakini

C. au

D. ili

26. Ni sentensi ipi iliyo sahihi kisarufi?

A. Watoto anacheza mpira sokoni.

B. Mtoto alienda sokoni

C. Watoto alipiga mpira

D. Mwanafunzi walienda sokoni



CamScanner

**27.** Chagua nomino dhahania

A. Hasira

B. Kalamu

C. Ndizi

D. Mto

**28. Kitenzi katika sentensi ifuatayo ni kipi?**

Mwanafunzi alikimbia haraka sana

A. Mwanafunzi

B. Haraka

C. Sana

D. Alikimbia

**29. Jaza nafasi iliyoachwa kwa kiambishi kifaacho**

Chumvi __mekolea kwenye mboga.

A. u

B. zi

C. li

D. i

**30. Kamilisha methali ifuatayo**

Akufaaye kwa dhiki, ___________

A. ndiye adui

B. ndiye rafiki

C. hakuchagulii tusi

D. hakuthamini



CamScanner

# TARGETER WINGS
# KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## GREDI YA 6 - MWAKA WA 2025
## SEHEMU B:
## KISWAHILI INSHA

Wings 005

*MUDA: Dakika 40*

| | |
|---|---|
| **JINA LAKO** | |
| **JINA LA SHULE YAKO** | |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**
2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

© *Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd Email:info@targeterpublishers.co.ke*



CamScanner

<u>*Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.*</u>

**Andika barua rasmi kwa Mwalimu ukiomba kujiunga na kikundi cha muziki shuleni mwenu.**



CamScanner